OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI
SHULE YA SEKONDARI IHALIMBA,
S.L.P 332,
MAFINGA

KUMB.NA.IHASS/FK I/VOL.01/14
MWANAFUNZI……
KIJIJI
CHA……
S.L.P …….
MAFINGA

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IHALIMBA MWAKA 2021

1. PONGEZI
   Ninayo furaha kukuarifu kuwa Umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza. Hongera sana, Shule ya Ihalimba ipo kijiji cha Vikula, Shule ina Hostel ya wasichana, Kuna nafasi chache kwa Wavulana. Ukiwa shuleni utajifunza na kufundishwa masomo Tisa (9) ya msingi yakiwemo SAYANSI masomo 3,HISABATI na Masomo ya SANAA matano(5) . Yote hayo yanafundishwa kwa KIINGEREZA isipokuwa somo la Kiswahili. Hivyo unatakiwa kujibidiisha sana katika kuelewa somo la kiingereza. Hilo ndilo Msingi wa Masomo mengine , Uje na Kamusi ya KIINGEREZA (DICTIONARY) kwa msaada zaidi.

2. KUFUNGUA KWA SHULE
   Shule itafungua tar 11/01/2021, fika bila kukosa au kuchelewa masomo yataanza saa
   1: 40 Asubuhi mchakamchaka ni saa 12: 30 Asubuhi.

3. MALENGO YA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI
   i. Lengo lako la Miaka 4 ni kuwa nani baada ya kuhitimu shule mfano Kuwa Daktari , Mwalimu, mwanasheria, Rubani, au Mkulima, nk
   ii. Utaonesha Mikakati mitatu (3) kufikia lengo lako karatasi la malengo limeambatanishwa Uje nalo.

4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

Sare ya shule (Vitambaa vimeambatanishwa)

A. WAVULANA

i. Suluali ya kaki moja- 1 bila malinda na turn up , upana wa miguu isiwe mfano wa chupa itachanwa.
ii. Suluali ya Dark blue -1 bila malinda na turn up upana wa miguu isiwe mfano wa chupa itachanwa.
iii. Shati Jeupe 1 Tetron lenye mikono mirefu na mikono mifupi 1
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vifupi jozi moja (1) vya kamba na Raba nyeupe Jozi 1
v. Sweta la kijani moja na dark blue moja zote mshono wa V
vi. Soksi jozi 2 nyeusi

B. WASICHANA

i. Sketi ya Kaki 1 na dark blue 1 linda boksi nyuma na mbele. Upana wa boksi sketi zote uwe nchi 7 na urefu nchi 9 kutoka kwenye magoti zaidi ya hapo sketi hazitapokelewa
ii. Shati jeupe moja tetroni mikono mirefu na mifupi 1
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vifupi jozi moja vyenye kamba na raba nyeupe jozi moja.
iv. Sweta la kijani moja na Dark blue moja zenye mshono wa V
v. Soksi jozi 2 nyeupe
vi. Hijabu nyeupe kwa Waislamu

NGUO ZA MICHEZO

- Traki dark blue jozi moja kwaajili ya kushindia na michezo
- Raba jozi moja
- T-shirt ya blue

MUHIMU: 1. Mwanafunzi harusiwi kuvaa sare iliyokuwa inatumika na mtu mwingine, sare zote vitambaa viwe namba 1 hii haipauki .

2. Nguo zote ziwekwe Alama ya jina lake maeneo ya mfukoni kwa wavulana na chini ya belti kwa wasichana.

5. MAHITAJI YA MWANAFUNZI

i. Daftari Kubwa 9 Quire 3 /4 na ndogo 9 kwaajili ya mazoezi.
ii. Karamu za wino na mkaa za kutosha
iii. Mathematical set 1 yaani Mkebe 1
iv. English Dictionary
v. Faili boksi dogo 1 kwaajili ya kuhifadhia Mitihani
vi. Begi la kubebea daftari.

VIFAA VYA USAFI

i. Ndoo ndogo lita 10
ii. Jembe kubwa 1

6:1 .SHERIA

Shule hii inaongozwa kwa mujibu wa ***sheria namba 25 ya mwaka 1978*** , aidha inaongozwa na taratibu , kanuni , miongozo , maagizo na maelekezo yatolewayo na wizara yenye dhamana nchini na ngazi zote. Unatakiwa kuzingatia mambo msingi yafuatayo

i. Heshima na utii kwa uongozi , wazazi , wafanyakazi, jamii na wanafunzi kwa kiwango cha juu.
ii. Mahudhurio ya vipindi vya darasani mwanzo hadi mwisho pamoja na shughuli zote za nje na ndani ya shule
    a. Lazima kuhudhuria Maandalizi yote ya jioni siku zote kuanzia saa 9: 20 hadi saa 11:45 na kuanzia saa 1: 30 had saa 4 :00 (**Evening preparation**)
iii. Ni lazima kuwahi siku zote shuleni na kanisani au Msikitini na kila siku saa 1:00 hadi 1:30 muda wa **SALA**
iv. Ni lazima ufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu kama mipaka yako iko ndani au nje ya shule
v. Ni lazima kutunza usafi wa mazingira na mwili wako kila siku
vi. Ni lazima kuvaa sare ya shule uwapo shule na utokapo nje ya shule kwa maelekezo
vii. Usipite jikoni au maeneo ya Hosteli kama siyo mhusika.
viii. Ni lazima uwe na faili moja kwaajili ya kuhifadhi mitihani yako yote.

6:2 . MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi wa aina yoyote ile
ii. Ukibainika unajihusisha na uasherati au mapenzi
iii. Ulevi, matumizi ya madawa ya kulevyana dawa za Kutoa mimba
iv. Makosa ya jinai kama kuua au kutishia kuua na kujiua
v. Kupiga au kupigana au kuchochea kupigana
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma kama kuvunja dawati ,kioo au mlango.
vii. Kuharibu au kudharau bendera ya Taifa
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
x. Kugoma , kuchochea au kuongoza migomo au kuvuruga usalama na amani ya shule
xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
xii. Kumiliki line au simu shuleni na kuwekeza simu mtaani.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. Fomu ya mwanafunzi kukubali nafasi na Tamko
2. Fomu ya mlezi/Mzazi ya kutoa ushirikiano
3. Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi yaani Fomu ya malengo ya mwanafunzi
4. Mwafunzi aletwe shuleni na mzazi au mlezi mweneyewe mapema.

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR- TAMISEMI)

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI IHALIMBA

S.L.P 332- MAFINGA.

1. FOMU YA MWANAFUNZI KUKUBALI NAFASI YA KUSOMA

Mimi…… ninakubali/ sikubali nafasi niliyopewa nipo tayari kusoma shule hii kuanzia 2021 hadi 2024 . Nitafuata sheria, taratibu, miongozo na maelekezo kwa mujibu wa wizara ya Elimu. Iwapo nitaenda kinyume nichukuliwe hatua zinazo stahili . Nakiri nimesoma na kuelewa fomu yangu ya kujiunga na shule. Ninaahidi kuwa mwanafunzi mtiifu kamwe sitavunja sheria nilizoziona katika fomu hii, na zile nitakazo pewa baada ya fomu hii. Sitaacha shule wala kumshawishi mwanafunzi yeyote kuacha shule.

Sahihi ya mwanafunzi……

tar……

2. FOMU YA MZAZI/MLEZI KUTOA USHIRIKIANO

Mimi……..mlezi au mzazi wa mwanafunzi…… nakubali / sikubali nafasi aliyopewa naahidi kutoa ushirikiano kwa mwanangu na uongozi wa shule kwa lolote lile katika malezi ya mwanangu , kimwili, kiroho na kitaaluma.Nitampa mahitaji yote kwa wakati ili kuongeza ufaulu wake katika Taaluma.Na akitoroka nitahusika kumtafuta kama hata patikana nichukuliwe hatua za kisheria .

Sahihi ya mzazi/mlezi……

tar……

3. FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI……JINSI……KABILA……
   TAREHE YA KUZALIWA……

2. JINA LA MZAZI BABA/ MLEZI…… JE YU HAI…….
   KAZI YAKE……NAMBA YA SIMU……..
   KIJIJI……KITONGOJI……..
3. JINA LA MZAZI MAMA/ MLEZI…… JE YU HAI……
   KAZI YAKE…… NAMBA YA SIMU .....……
   KIJIJI……KITONGOJI……..…
4. JINA LA NDUGU WAWILI (
   a)……simu…….
   (b)……simu……
   ……
5. HISTORIA YA MWANAFUNZI. Hali yake ya kiafya tangu anapokuwa ipoje? Eleza kwa ufupi ili
   usaidiwe……
   ……..

MAHITAJI YA WANAFUNZI

i. Gauni Maruni mshono wa solo lenye mkanda mweusi kitambaa kizito refu na wavulana suluali nyeusi na T-Shirt ya blue
ii. Sahani, bakuli na kikombe VYOTE VIWE VYA BATI .
iii. Nguo za ndani za kutosha .

MUHIMU: USIMTANGULIZE MTOTO KUKAA HOSTELI KABLA YA MALIPO TUTASHINDWA KUMHUDUMIA.

KARIBU SANA

MPELEKE MTOTO SHULENI , LEO AJE ATATUE CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA FAMILIA, KATA, WILAYA , MKOA NA TAIFA.

L.S. Shayo

LIZA SOSTEN SHAYO -0763069567

MKUU WA SHULE